# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 028

APRILI- JUNI, 2025


# RAIS DKT. SAMIA AZINDUA MRADI WA MAJI LAMADI WA BILIONI 12, AWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA BILIONI 440 SIMIYU



# RAIS DKT. SAMIA AZINDUA MRADI WA MAJI LAMADI WA BILIONI 12, AWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA BILIONI 440 SIMIYU

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameandika historia mpya katika Sekta ya Maji nchini kwa kufanya uzinduzi wa Mradi wa Maji wa Lamadi wenye thamani ya Shilingi bilioni 12.83 na kuweka jiwe la msingi kwa Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wenye thamani ya Shilingi bilioni 440, yote mkoani Simiyu.



Katika hafla hiyo ya kihistoria Rais Samia amesema kuwa utekelezaji wa miradi hiyo miwili utaboresha kwa kiwango kikubwa huduma ya majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira kwa wakazi wa miji ya Lamadi na Nyashimo kwa Mradi wa Lamadi, pamoja na Busega, Itilima, Bariadi, Lagangabilili na vijiji 103 kwa awamu ya kwanza ya Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

"Ninaamini kuwa ujenzi wa mradi wa Lamadi niliouzindua, na huu niliouwekea jiwe la msingi hapa Nyashimo kwa pamoja itaboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mkoa wetu wa Simiyu," Rais Samia amesema.

Rais Samia ameitaka Wizara ya Maji kuendelea kushirikiana na viongozi wa mikoa ili kufanikisha mpango wa kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi.

Aidha, Rais Samia ametoa shukrani kwa wadau wa maendeleo ambao ni Mfuko wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund - GCF), Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) ambao wanashirikiana nasi katika utekelezaji wa mradi huo mkubwa kwa gharama ya Shilingi Billion 440.

Pia, ametoa shukurani kwa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank- EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) ambao wamegharamia ujenzi wa mradi wa maji Lamadi kwa gharama ya Shilingi Bilioni 12.83. Akisisitiza ushirikiano wao umekuwa muhimu kufanikisha miradi hiyo ya kimkakati

Katika hatua nyingine, Rais Samia ameagiza juhudi za kuhifadhi mazingira ziendelee kufanyika kikamilifu kwa kushirikisha sekta zote kwa kuwa uhifadhi wa mazingira ni msingi wa uendelevu wa upatikanaji wa maji, kuwezesha shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwemo kilimo, viwanda, ufugaji, uvuvi na utalii.





Mradi wa Maji wa Lamadi ni sehemu ya Satellites Town Projects ambapo awali, mradi huo ulikuwa na lengo la kuhudumia wakazi 27,000, lakini kwa sasa unahudumia zaidi ya wakazi 85,000 katika kata za Lamadi, Mkula na Lutubiga baada ya kupanua miundombinu ya usambazaji na kuongeza uwezo wa pampu, huku uzalishaji wa maji ukifikia lita milioni 33 kwa siku dhidi ya mahitaji ya lita milioni 24.2.

Kwa upande wa Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi unalenga kuhudumia wakazi wapatao 495,000 katika wilaya tano za Simiyu ambazo ni Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu. Unahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Bariadi, Busega, Itilima na vijiji 103, pamoja na miradi ya kilimo himilivu na uhifadhi wa mazingira unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2025.

Hii ni historia kwa Rais Samia kutekeleza hatua hizo mbili kubwa kwa Sekta ya Maji katika mkoa mmoja ndani ya siku moja, jambo linaloonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kusogeza huduma ya maji kwa wananchi. Upatikanaji wa maji kwa sasa katika Mji wa Lamadi umefikia asilimia 97 na kufanya lengo la Serikali la kufikia lengo la zaidi ya asilimia 95 ya upatikanaji wa maji safi na salama Mijini

Awali, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema kuwa kati ya vijiji 12,318 vilipo nchini vijiji 10,779 vimefikiwa na huduma ya maji na vijiji 1,539 vilivyobaki vinataegemewa kufikiwa baada ya kukamilika kwa miradi mikubwa ya kimkakati ikwemo mradi huu wa Simiyu na miradi mingine inayoendelea kutekelezwa nchini kote.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri amesisitiza Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara, mkoa, halmashauri na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ili kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji nchini.

# RAIS DKT. SAMIA AAGIZA ZIWA VICTORIA KUTUNZWA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema utekelezaji wa miradi yote ya maji imelenga kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, lakini pia ni muhimu kulinda mazingira ya Ziwa Victoria ambalo ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya kibiashara katika Jiji la Mwanza na maeneo jirani.

Rais Dkt. Samia ametoa agizo hilo mara baada ya kuzindua rasmi Mradi wa Chanzo cha Maji Butimba, wenye thamani ya Shilingi Bilioni 71.6, akisema kuwa mradi huo utaboresha kwa kiwango kikubwa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wakazi wa Mwanza na maeneo jirani.

“Maziwa Makuu ikiwemo Ziwa Victoria ni vyanzo vya uhakika vya maji kwa matumizi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii, hivyo niwakumbushe kuwa suala la uhifadhi wa mazingira ikiwemo kudhibiti kuenea kwa magugu maji katika Ziwa Victoria ni msingi wa uendelevu wa upatikanaji wa maji, kuwezesha shughuli mbalimbali za maendeleo kama vile kilimo, viwanda, ufugaji, uvuvi, utalii na usafiri kwa njia ya maji,” Rais Samia amesema.

“Kwa muktadha huo, Naagiza juhudi za kuhifadhi mazingira ziendelee kufanyika kikamilifu kwa kushirikisha sekta zote,” Rais Samia ameagiza
Aidha, Rais Dkt. Samia amefurahishwa na mradi kuhusisha ujenzi wa vyoo vya kisasa vya umma vipatavyo 107 katika mashule, zahanati na masoko katika Wilaya za












Nyamagana na Ilemela. Akisema kuwa ni dhahiri kuwa programu hii ya LVWATSAN imegusa maisha ya kila siku ya wananchi wa Jiji la Mwanza.
Pia, Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa Mradi huu umetekelezwa kupitia Programu ya Lake Victoria Water and Sanitation (LVWATSAN) kwa ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank - EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Agence Française de Développement - AFD). Akitoa shukrani kwa Washirika na Wadau wa Maendeleo kwa ushirikiano wao na Serikali katika kuleta maendeleo.

Rais Dkt. Samia amesema kuwa kupitia programu ya LVWATSAN awamu ya kwanza, miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya namna hii imetekelezwa na kukamilika katika Miji ya Magu na Misungwi Mkoani Mwanza, pamoja na Mji wa Lamadi uliopo Wilaya ya Busega Mkoani Simiyu ambao ameuzindua siku ya jana.

Awali, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema kuwa kabla ya mradi huu, Jiji la Mwanza lilikuwa likitegemea chanzo cha Capripoint chenye uwezo wa kuzalisha lita 90,000,000 kwa siku wakati mahitaji yalikuwa ni lita 188,000,000. "Kupitia mradi wa Butimba, uzalishaji umeongezeka hadi kufikia lita 138,000,000 kwa siku, hatua ambayo imepunguza migao ya maji na kuongeza muda wa upatikanaji wa huduma," Waziri Aweso amesema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, amefafanua kuwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa Jiji la Mwanza mwaka 2021 ilikuwa wastani asilimia 63.15, hivi sasa upatikanaji wa maji umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 87, ongezeko hili limechangiwa na kukamilika kwa miradi ya usambazaji maji ukiwemo ujenzi wa chanzo cha Butimba. Aidha, amesisitiza matarajio ya Wizara ya Maji ni kufikia wastani wa asilimia 98 mwezi Desemba 2026 baada ya mradi wa usambazaji kukamilika.

Maeneo yanayofaidika na mradi huu ni pamoja na Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Nyamazobe, Nyahingi, Buganda, Luchelele, Lwanhima, Sahwa, Fumagila, Kishiri na Igoma katika Jiji la Mwanza, pamoja na maeneo ya Kisesa, Bujora na Kanyama katika Wilaya ya Magu.

Dodoma, Siku ya Mazingira Duniani

Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philipo Isdory Mpango akiwa katika Banda la Wizara ya Maji kujionea hatua mbalimbali zinazochukuliwa za kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi.

Mhe. Dkt. Mpango amemwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Siku ya Mazingira Duniani, jijini Dodoma.





# Serikali inaendelea na kazi ya utekelezaji wa miradi ya maji ili kuwafikia wananchi wote.



Waziri mkuu Mhe. Kassim Majaliwa amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika maeneo yote nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo katika makazi yao.

Amesema hayo wakati akizungumza na wananchi katika eneo la Hungumalwa wilayani Kwimba, Mwanza baada ya kuzindua mradi wa maji Hungumalwa.

Mhe.Majaliwa amewasisitiza wananchi kuendelea kuiamini na kushirikiana na Serikali ambayo imedhamiria kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Tutaendelea kusimamia maelekezo ya Rais Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan na tutaendelea kutekeleza ilani kwa vitendo. Tutawahudumia wananchi wala msiwe na mashaka. Suala la maji tunaendelea kuhakikisha yanapatikana maeneo yote."

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoa wa Mwanza, Mhandisi Godfrey Sanga amesema gharama ya mradi ni shilingi bilioni 11, na mpaka sasa kazi zote zimekamilika kwa thamani ya shilingi bilioni 10 hivyo kubakiza salio katika mkataba wa ujenzi wa mradi kiasi cha shilingi milioni 201.

Ametaja kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa tangi moja la ujazo wa lita milioni moja, ununuzi wa mabomba na viungio vyake km 54.817, uchimbaji na ufukiaji mitaro yenye urefu wa km 54.817, kuunganisha maji kwa wateja wa majumbani 500, ujenzi wa ofisi ya Chombo cha Watumia Maji ngazi ya Jamii na ujenzi wa nyumba ya mlinzi, ambapo kazi zote zimekamilika.

Mradi huo ulianza kutekelezwa tarehe 8 Machi 2022 na kukamilika tarehe 15 Agosti 2024



# DKT.. BITEKO AWATAKA WATANZANIA KUTOGAWANYIKA WAKATI WA UCHAGUZI MKUU

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewataka wananchi kutogawanywa kwa itikadi ya dini wala siasa wakati huu kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Ubunge na Udiwani kwa manufaa ya Taifa.

Dkt. Biteko amesema hayo wilayani Monduli mkoani Arusha wakati akizungumza na wananchi mara baada ya kuzindua mradi wa maji katika Kijiji cha Esilalei.

“ Ninatamani kuona hatugawanyiki na mtu yoyote wala hatuwekwi kwenye makundi ya dini wala ukabila. Nataka niwaombe wananchi wa Monduli pendaneni na shirikianeni na uchaguzi utakapofika chaguaneni kwa haki,” amesema Dkt. Biteko.

Amewataka wananchi wa Monduli kuutunza mradi huo wa maji wa Esilalei “ Nawapongeza Wizara ya Maji na RUWASA kwa kusimamia mradi huu mzuri na wa uhakika, bila shaka mtaona itakapofika Desemba mwaka huu awamu ya pili ya mradi itakuwa imekamilika,”

Pia, Dkt. Biteko amesema kuwa Serikali inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inawapenda wananchi wa Monduli na inawapongeza kwa uchapakazi wao kwenye kilimo na ufugaji.

Aidha, amewataka wachape kazi na kuwa Rais Samia amefikisha mradi huo wa maji kwa kuwa anapenda pia mifugo yao istawi.vilevile, amesema kuwa Rais Samia amemtuma kuwahakikishia wananchi hao kuwa wafugaji nchini wanakuwa daraja la juu kama walivyo wananchi wengine.

Aidha, amesema wananchi hao wanachohitaji ni Serikali iwapatie nyenzo kama maji, umeme na barabara ili kufanikisha shughuli zao ambapo tayari Rais Samia ameapa kuwapatia nyenzo hizo.

Naibu Waziri wa Wizara ya Madini Dkt. Steven Kiruswa amefurahishwa kwa Wilaya hiyo kupata maji na kusema kuwa maji ni uhai, hivyo anamshukuru Rais Samia kwa kusaidia pia mifugo kupata maji.

Mbunge wa Monduli, Mhe. Freddy Lowasa amesema kuwa kazi aliyofanya Rais Samia wilayani humo ni kubwa kwa kuwa huduma ya maji ilikuwa changamoto kubwa kwao.

“ Kwa miaka mingi maji yamekuwa kero kubwa katika Wilaya yetu kwa kupata mradi huu tunaomba umpelekee shukrani zetu Rais Samia,” amesema Mhe. Lowassa.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Monduli, Mhandisi Naville Msaki amesema kuwa mradi huo ulisanifiwa mwaka 2021 utahudumia wananchi 8,867 na mifugo 24,000 na umefikia asilimia 96 na hadi kukamilika kwake utagharimu shilingi bilioni 2.7.

# Mwasenkwa jijini Mbeya wapata neema ya maji



Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Mabunge duniani amezindua mradi wa maji wa kisima katika Kata ya Mwasenkwa Jijini Mbeya, katika mtaa wa Mwazumbo.. Mradi huo umetelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya UWSA).
Katika hafla hiyo, Dkt. Tulia amesema Serikali inapambana kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi ikiwemo huduma ya maji, hivyo uzinduzi wa mradi huu ni mwendelezo wa ahadi ya Serikali ya kumtua mama ndoo kichwani na kuwataka Wananchi kuunga mkono juhudi hizo kwa kutunza vyanzo vya maji na kuacha kufanya shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji.

Aidha, ameipongeza Mbeya UWSA kwa kuendelea kubuni miradi ya kuboresha huduma ya maji katika maeneo yenye upungufu wa huduma
.
Akitoa salamu Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya UWSA CPA. Gilbert Kayange, amesema Mamlaka imeendelea kubuni, kusanifu na kutekeleza miradi ya maji kwenye maeneo mbalimbali kwa lengo la kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo hayo.

CPA. Kayange amesema kupitia mpango huo miradi mbalimbali ya maji imekamilika na imeanza kutoa huduma, ikiwemo mradi wa maji wa Mto Simba ambao unanufaisha wananchi wa Kata ya Tembela na Mwasanga, mradi wa maji wa kisima cha Gombe ambao unahudumia wakazi wa Gombe kusini na mradi wa maji wa Kisima cha Mwenge ambao unahudumia wananchi wa Mtaa wa Mwenge na maeneo ya jirani.

CPA. Kayange amesema Mamlaka itaanza utekelezaji wa miradi mingine ya kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya Itende, Nsalaga, Sinde, Itezi, Uyole, Kalobe, Isanga na Inolo.
Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi, Mhandisi Barnabas Konga, Mkurugenzi wa Uzalishaji Maji na Usafi wa Mazingira amesema, utekelezaji wa mradi wa kisima cha Mwasenkwa ulianza Januari



2025 na kukamilika mwezi Machi 2025 kwa gharama ya Shilingi Milioni 123.
Mradi huo unazalisha maji Lita 720,000 kwa siku na ananufaisha zaidi ya wananchi elfu mbili kata ya Mwasenkwa.

# Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2025/2026. Ufuatao ni muhtasari wa Bajeti hiyo;

## MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MAJI KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA (2020/21 – 2024/25)



1. Kipindi cha miaka minne (4) cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mafanikio mengi yamepatikana kwenye sekta ya maji. Ninaomba nitumie fursa hii kutaja baadhi ya mafanikio hayo kama ifuatavyo: -

(i) Kukamilika na kuridhiwa kwa Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, Toleo la Mwaka 2025. Sera hiyo inaelekeza Wizara ya Maji kuratibu na kuwa na mipango ya pamoja na sekta nyingine zinazotekeleza miradi inayohusu maji ikiwemo sekta binafsi.

(ii) Utekelezaji wa miradi ya maji:

a) Jumla ya miradi ya maji 2,612 imekamilika (vijijini 2,331 na mijini 281) na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asilimia 83 mwezi Desemba, 2024 na maeneo ya mijini kutoka wastani wa asilimia 84 hadi asilimia 91.6. Baadhi ya miradi iliyokamilika ni awamu ya kwanza ya mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda miji ya Tinde na Shelui; mradi wa ujenzi wa mfumo wa kutibu maji katika Mji wa Bunda; mradi wa ujenzi wa chanzo cha maji Butimba; mradi wa maji Kyaka/Bunazi mkoani Kagera; mradi wa maji katika Mji wa Orkesumet; mradi wa maji Dareda, Singu, Sigino na Bagara mkoani Manyara; na miradi 218 chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19.

b) Kukwamuliwa kwa miradi iliyochukua muda mrefu kujengwa ikiwemo miradi ya Same-Mwanga-Korogwe; Bunda; Mugango, Kiabakari hadi Butiama; ujenzi wa tekeo la maji katika Mji wa Kigoma; na miradi ya maji 177 katika maeneo ya vijijini maarufu kama miradi chechefu.

c) Kuanza kwa utekelezaji wa miradi ya maji ya kimkakati ikiwemo mradi wa maji wa miji 28; ujenzi wa bwawa la Farkwa; mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Simiyu; mradi wa maji kutoka Kahama kwenda Halmashauri ya Ushetu; mradi wa kutoa maji Dambia kwenda Hydom; mradi wa maji Ukirigulu, Koromije hadi Sumve; na mradi wa uboreshaji miundombinu ya maji na utunzaji wa mazingira Jijini Tanga pamoja na miji ya Muheza, Pangani na Mkinga.

(iii) Kuongezeka kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira:

a) Bajeti ya Wizara kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 680 mwaka 2021/22 hadi zaidi ya Shilingi trilioni moja hivyo kuchochea kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini. Ongezeko hili linahusisha matumizi ya fedha za ndani kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo miradi ya maji ya bwawa la Kidunda na Mradi wa Maji wa Tunduma-Vwawa.

b) Kuongezeka kwa fedha za utekelezaji wa Programu ya Maji ya Malipo kwa Matokeo (PforR) inayofadhiliwa na Benki ya Dunia kutoka Dola za Marekani milioni 350 hadi Dola za Marekani milioni 654. Aidha, ongezeko hili limetokana na Tanzania kuwa kinara miongoni mwa nchi zinazotekeleza Programu hiyo.

c) Kupata chanzo kipya cha fedha kupitia mauzo ya Hati Fungani ya Kijani yenye thamani ya Shilingi bilioni 54.72.

(iv) Kuboreshwa kwa mazingira ya kazi ya watumishi baada ya kukamilika kwa ujenzi wa ofisi ya Wizara ya Maji na baadhi ya taasisi zake na ununuzi wa samani. Aidha, Serikali imeendelea kununua vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri, magari ya kuondosha majitaka, seti 25 za mitambo ya uchimbaji wa visima na seti tano (5) za mitambo ya ujenzi wa mabwawa.

(v) Kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa 45 madogo na ya ukubwa wa kati kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

(vi) Kuboreshwa kwa matumizi ya mifumo ya TEHAMA iliyowezesha uwazi na uwajibikaji katika makusanyo na matumizi ya maduhuli yatokanayo na huduma za maji.

(vii) Kuanza kutumika kwa dira za maji za malipo ya kabla ya matumizi kwa wananchi na taasisi hivyo kuboresha huduma ya maji, kupunguza malalamiko ya wateja kwenye ankara za maji na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli.

(viii) Chuo cha Maji, kuongeza udahili kutoka wanafunzi 2,320 hadi 4,260 sawa na ongezeko la asilimia 84; kufanya tafiti na kutoa machapisho ya kisayansi 52; na kuanzisha Consultancy Bureau inayosaidia kujenga uwezo kwa vijana wanaohitimu.

(ix) Mfuko wa Taifa wa Maji umeendelea kuzijengea uwezo Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji katika kuandaa maandiko ya miradi kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha ambapo kiasi cha Dola za Marekani Milioni 9.3 zimepatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, kupitia dirisha lake la mikopo ya riba nafuu (revolving fund), Mfuko unatoa mikopo kwa mamlaka za maji nchini.

(x) Mafanikio katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ni pamoja na kuimarika kwa utunzaji na uendelezaji wa vyanzo vya maji ambapo jumla ya vyanzo 68 vimetangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu kutoka vyanzo 18 vilivyokuwepo mwaka 2021; na kutekelezwa kwa Mipango ya Uhifadhi wa Vidakio vya Maji ambayo imewezesha kupandwa kwa miti rafiki wa maji 3,715,838.

(xi) Mafanikio kwa upande wa ubora wa maji ni pamoja na kuimarika kwa huduma za ubora wa maji kutokana na kujengwa kwa maabara ya Manyara hivyo kuwa na jumla ya maabara za maji 17. Aidha, Maabara sita (6) za Singida, Shinyanga, Kigoma, Bukoba, Musoma na Dar es Salaam zimejengewa uwezo na kupata ithibati hivyo kufanya maabara zinazoweza kuzalisha takwimu zinazokubalika kimataifa kufikia saba (7) kutoka moja ya Mwanza iliyokuwepo mwaka 2021.

(xii) Kuimarika kwa uhusiano na ushirikiano na wadau wa maendeleo hususani wa nje hivyo, kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi pamoja na ushauri wa kitaalam.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

2.1.1. Upatikanaji wa Fedha

2. Mwaka 2024/25, Fungu 49 liliidhinishiwa Shilingi bilioni 627.78 ambapo Shilingi bilioni 69.66 ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 558.12 ni za maendeleo. Hadi mwezi Aprili, 2025, Wizara imepokea Shilingi bilioni 528.39 sawa na asilimia 84.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi bilioni 479.94 ni za maendeleo na Shilingi bilioni 48.44 ni za matumizi ya kawaida.

2.1.2. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

3. Shilingi bilioni 69.66 zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2024/25, Shilingi bilioni 52.12 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji na Shilingi bilioni 17.54 ni za matumizi mengineyo. Hadi mwezi Aprili, 2025 Shilingi bilioni 48.44 sawa na asilimia 69.5 zimetolewa ambapo Shilingi bilioni 38.62 ni za mishahara na Shilingi bilioni 9.82 ni za matumizi mengineyo.

2.2. Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

4. Upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka 2024/25, Fungu 49 lilitengewa Shilingi bilioni 558.12. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 340,463,656,000.00 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 217,651,723,000.00 ni fedha za nje. Hadi mwezi Aprili 2025, Wizara imepokea Shilingi bilioni 479,948,853,338.37 sawa na asilimia 86 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi bilioni 378,646,432,010.26 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 101,302,421,328.11 ni fedha za nje. Aidha, fedha hizo zimetumika kulipa hati za madai ya watoa huduma na vilevile, wale waliowasilisha madai wanaendelea kulipwa. Aidha, wakati wa utekelezaji wa bajeti, Wizara iliomba uhamisho (Realocation) wa fedha za maendeleo za ndani kwa ajili ya kulipa madai ya wakandarasi na watoa huduma wengine na hivyo kuongeza bajeti ya fedha za ndani

2.3. Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo

5. Mwaka 2024/25 utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo umeainishwa katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira; na kazi mbalimbali zinazotekelezwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara; na masuala mtambuka.

2.3.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji na Ubora wa Maji

6. Uendelezaji wa rasilimali za maji, Wizara imekamilisha ujenzi na ukarabati wa mabwawa madogo na ya ukubwa wa kati matano (5) ya Ipililo, Lalago, Misigiri, Utyatya na Nyanja-Salama. Vilevile, vyanzo 894 vilihakikiwa ubora wake na matokeo yanaonesha hali ya ubora wa maji katika vyanzo inalinda afya ya ikolojia na vyanzo hivyo vinaweza kuendelezwa kwa matumizi mbalimbali. Aidha, skimu 1,288 za maji vijijini na mijini zilihakikiwa na kukidhi ubora.

2.3.2. Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

7. Hadi mwezi Aprili 2025, miradi 463 yenye jumla ya vituo 4,484 imekamilika na inahudumia wananchi 3,170,769. Aidha, miradi mingine inaendelea na utekelezaji ikiwemo mradi wa maji Ruangwa, Lindi na Nachingwea. Awamu ya kwanza inahusisha kupeleka maji kwenye vijiji 29 na utekelezaji umefikia asilimia 60 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26.

8. Miradi mingine inayotelekezwa ni Mkinga – Horohoro ambao hadi mwezi Aprili 2025, utekelezaji umefikia asilimia 45 na utanufaisha wananchi 74,795 wa Mji wa Horohoro na vijiji 37 vya Wilaya ya Mkinga. Vilevile, kuna mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Usagara, Ukiliguru, Sumve hadi Koromije na vijiji 24 vya Wilaya za Misungwi na Kwimba ambapo utekelezaji umefikia asilimia 32 na utanufaisha wananchi 162,377.

9. Programu ya kupeleka huduma ya maji kwenye vijiji visivyo na huduma maarufu kama Programu ya Visima 900 inahusisha uchimbaji wa visima vitano (5) na ujenzi wa point source katika kila Jimbo la Uchaguzi. Aidha, baadhi ya maeneo kwenye majimbo yaliyokuwa na vyanzo vingine kama chemchemi, mito na mabomba ya maji, vimetumika kama vyanzo mbadala. Hadi mwezi Aprili 2025, jumla ya visima vilivyochimbwa pamoja na vyanzo mbadala vinavyoendelezwa ni 702. Kazi inayoendelea ni ujenzi wa point sources ambapo 460 zimekamilika na zinatoa huduma ya maji. Wizara inaendelea na utafiti wa maji kwenye vijiji vingine ikiwemo vile ambavyo visima vyake vilikosa maji.

2.3.3. Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

10. Wizara imeendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo ya mijini ambapo miradi 68 yenye uwezo wa kuhudumia wananchi 3,362,850 imekamilika.

11. Hadi mwezi Aprili 2025, baadhi ya miradi iliyokamilika ni pamoja na: -

Mradi wa ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji na matanki ya kuhifadhia maji Kusini mwa Dar es Salaam na unahudumia wananchi wapatao 450,000 wa maeneo ya Bangulo, Mwanagati, Kitunda, Kipunguni, Majohe, Kivule, Magole, Msongola, Chanika na Chalambe; Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari – Butiama na unahudumia zaidi ya wananchi 100,000; na Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe uliozinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 9 Machi, 2025 na unahudumia wananchi wapatao 456,900.

12. Aidha, kuna miradi 226 inayoendelea na utekelezaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo:-



(i) Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Mbeya kupitia chanzo cha Mto Kiwira;

(ii) Mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Jiji la Dodoma kwa maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Chamwino;

(iii) Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Mwanza maeneo ya Kisesa, Buswelu, Luchelele pamoja na Wilaya za Ilemela, Magu na Misungwi;

(iv) Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Manispaa ya Morogoro utakaonufaisha wananchi wa maeneo ya Mindu, Mikoroshini, Mkwajuni, Madaganya, Kingolwira, Misongeni na Kitungwa;

(v) Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu utakaonufaisha wananchi wa Wilaya za Bariadi, Busega, Itilima, Meatu na Maswa; na

(vi) Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ya: Handeni, Korogwe, Muheza, Pangani, Kilwa Masoko, Nanyumbu, Ifakara, Rujewa, Chunya, Njombe, Makambako, Wanging'ombe, Kiomboi, Singida, Manyoni, Mugumu, Chemba, Chamwino, Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo, Kaliua, Kayanga, Chato, Geita, Newala, Nanyamba, Tandahimba, Mafinga, Rorya, Tarime, Songea na sehemu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.

# VIPAUMBELE NA MPANGO KWA MWAKA 2025/26

4.1 Vipaumbele vya Sekta ya Maji
13. Mwaka 2025/26, Wizara imeweka vipaumbele vinavyozingatia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Kutekeleza miradi ya maji 1,539 inayoendelea ambapo miradi 1,313 inatekelezwa vijijini na miradi 226 mijini ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati katika maeneo mbalimbali nchini;

(ii) Kukamilisha Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji (National Water Master Plan);

(iii) Kuimarisha uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na uendelezaji wa vyanzo vya maji ikiwemo uchimbaji wa visima na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua;

(iv) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa ubora wa maji kwa kuhakikisha yanakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa;

(v) Kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma endelevu pamoja na kudhibiti upotevu wa maji; na

(vi) Kutekeleza miradi ya gridi ya taifa ya maji ikiwemo mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda miji ya Dodoma na Singida; mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kwenda Kigoma, Katavi na Rukwa; mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kwenda Mtwara na Lindi; mradi wa kutoa maji Mto Rufiji kwenda mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; na miradi ya kutoa maji maziwa ya Victoria na Nyasa kwenda maeneo mbalimbali ikiwemo vijiji vilivyo jirani na maziwa hayo.
4.2 Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26
14. Mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26 umezingatia maeneo yafuatayo: -
4.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji na Ubora wa Maji
15. Mwaka 2025/26 Wizara imepanga kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji pamoja na ubora wa maji; na kutekeleza jumla ya miradi 1,539 ya majisafi na usafi wa mazingira ambapo miradi 1,313 ni ya vijijini na 226 ni ya mijini.

4. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26
16. Ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi trilioni moja, bilioni kumi na sita, milioni mia nane tisini na nne, laki tisa hamsini na nane elfu (Shilingi 1,016,894,958,000) kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2025/26, ambapo Shilingi 73,779,579,000 ni za matumizi ya kawaida na Shilingi 943,115,379,000 ni za maendeleo.

17. Fedha za matumizi ya kawaida, Shilingi 18,081,382,000 ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo (OC) na Shilingi 55,698,197,000 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi (PE) wa Wizara, RUWASA, Mfuko wa Taifa wa Maji na Chuo cha Maji. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Shilingi 340,463,656,000 sawa na asilimia 36.1 ni fedha za ndani na Shilingi 602,651,723,000 sawa na asilimia 63.9 ni fedha za nje.

18. Hotuba inapatikana katika tovuti ya Wizara yenye kikoa cha www.maji.go.tz









# Dodoma, Maadhimisho ya Wiki ya Mazingira







Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ametembelea mabanda yanayoonesha hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika utunzaji wa mazingira, ikiwemo banda la Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira pamoja na banda la Wizara ya Maji likihusisha taasisi mbalimbali zikiwemo Maabara za Ubora wa Maji, Bodi ya Maji Bonde la Wami/ Ruvu, Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA)

# VIFAA VYA UTAFITI WA MAJI CHINI YA ARDHI VYAONGEZWA



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amewataka wataalamu wa Mabonde kujikita katika kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi ili huduma ya maji kwa wananchi iwe endelevu.

Mhe. Aweso ameyasema hayo wakati akikabidhi vifaa vya kisasa vya utafiti wa maji chini ya ardhi vilivyonunuliwa kwa fedha za UVIKO.

“Vifaa hivi viwe chachu ya kuwaongezea uwezo wataalamu wetu na kuweka nguvu katika utafiti ili maeneo yaliyokuwa na changamoto ya upatikanaji wa maji yapate maji” Waziri Aweso amesema ambapo vifaa hivyo vinagawanywa katika mabonde tisa ya maji.

Mkurugenzi wa Idara ya Rasilimali za Maji Dkt. George Lugomela amesema vifaa hivyo vitawezesha kuchunguza uwepo wa miamba inayohifadhi maji kwa ufanisi hadi kina cha urefu wa mita 1000.


Vifaa hivyo ni pamoja na kifaa cha kuchunguza mipasuko katika miamba kwa njia ya sumaku (Magnetrometer), kifaa cha kuchunguza maji (terrameter),kifaa cha kupima kina cha maji (deeper),kifaa cha kuchunguza mikondo ya maji



na kifaa cha kuchukua majira (GPS).

Mkurugenzi Lugomela amemshukuru Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwezesha kwa fedha zinazosaidia kufikisha azma ya kupata huduma ya maji kwa wananchi kwa asilimia 85 vijijini na 95 mjini ifikapo 2025.

# Waziri Aweso Akagua Ujenzi wa Ofisi za RUWASA, Agawa Magari 19 kwa Ofisi za Makao Makuu na Wilaya.



Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso, amekagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) na kukabidhi magari 19 kwa ajili ya ofisi za makao makuu na wilaya mbalimbali nchini. Akizungumza mara baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi huo, Waziri Aweso alisema RUWASA ilianzishwa kutokana na changamoto kubwa ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini, jambo lililopelekea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, kuona umuhimu wa kuanzishwa kwa wakala huo.

“Leo hii suala la ujenzi wa miradi ya maji vijijini siyo tatizo tena. Namshukuru sana Rais Samia kwa kuwa ujenzi wa taasisi hii unaenda sambamba na mazingira bora ya kazi kwa watumishi,” alisema Waziri Aweso.

Ameeleza kuwa Rais Samia alitoa kiasi cha Shilingi bilioni 24 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya RUWASA, na kupongeza juhudi hizo akisema: “Hakika Rais wetu ni mjenzi. Yote aliyotufanyia tutamlipa kwa kufanya kazi kwa bidii, kwani amefanya kazi kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini.”

Ameongeza kuwa watahakikisha wanamfuatilia mkandarasi kwa karibu ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati, na fedha zitatolewa kwa wakati ili kuondoa changamoto au malalamiko yoyote.

“Ujenzi bora wa miradi ya maji unaendana na usimamizi makini na ufuatiliaji wa karibu. Nitahakikisha RUWASA wanapata ushirikiano wote wanaouhitaji ili kukamilisha yote waliyokusudia,” alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya RUWASA, Bi. Ruth Koya, alimshukuru Waziri Aweso kwa kuonesha uangalizi wa kipekee kwa taasisi hiyo, akisema magari 19 yaliyotolewa yataongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya RUWASA.

“Rais Samia Suluhu Hassan aliahidi kumtua mama ndoo kichwani na anaendelea kutekeleza hilo kwa vitendo. Waziri wa Maji naye anatekeleza wajibu wake kwa dhati. Magari haya yatasaidia kufanikisha lengo la Ilani ya CCM ya kuhakikisha huduma ya maji vijijini inafikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025,” alisema.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Kitengo cha Ushauri Elekezi wa mradi huo, Bw. Peter Salyeem, aliwasilisha taarifa ya maendeleo ya ujenzi, akieleza kuwa mchakato ulianza Machi 2022 kwa maandalizi ya michoro, tathmini ya gharama na mazingira. Ujenzi ulianza rasmi Novemba 2023.

Alieleza kuwa mradi huo unagharimu Shilingi bilioni 24.9, huku gharama za ushauri elekezi zikiwa Shilingi milioni 499. Fedha zote zinatolewa na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Maji.

“Mradi huu unahusisha ujenzi wa jengo kuu la ofisi ya RUWASA, kazi za nje, majengo saidizi kama mgahawa, kibanda cha mlinzi, jengo la jenereta pamoja na uzio wa eneo lote la kiwanja,” alisema.

Alibainisha kuwa mkandarasi wa mradi ni kampuni ya China Jiangxi International Economic and Technical Company Limited, huku mshauri elekezi akiwa ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 12, kuanzia Novemba 2023 hadi Desemba 31, 2024, na hadi sasa umefikia asilimia 70 ya utekelezaji.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu kutoka RUWASA, Bw. Titus Mkapa, alithibitisha kuwa magari yaliyokabidhiwa ni 19 na yataelekezwa kwenye ofisi za makao makuu pamoja na wilaya ili kuongeza ufanisi wa shughuli za utoaji huduma za maji vijijini.

# Zanzibar wapigwa msasa kuhusu rasilimali za maji




Wataalamu wa Sekta ya Maji wa Tanzania Bara wamewapitisha wenzao kutoka Zanzibar kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji na usafi wa mazingira.

Wataalamu hao wanatoka Wizara ya Maji,Nishati na Madini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mafunzo yamefanyika katika ofisi za Wizara ya Maji, Mtumba jijini Dodoma.

Lengo la mafunzo ni kujenga uelewa kuhusu namna sahihi ya uendeshaji na miongozo kuhusu usambazaji na usimamizi wa rasilimali za maji na usafi wa mazingira baada ya mabadiliko ya sera ya maji,2025.

Kupitia sera hiyo Wizara ya Maji.,Nishati na Madini Zanzibar inategemea kubadilisha jina na majukumu ya Idara ya Maendeleo ya Maji na kuwa Idara ya Maendeleo ya Maji na Usafi wa Mazingira ambayo itakuwa na mgawanyo kuhusu Usimamizi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira na Usimamizi wa Rasilimali za maji.

Mafunzo hayo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji ,Mkurugenzi Ifara ya Sera na Mipango Prosper Buchafwe ndc amebainisha mafanikio yaliyopatikana katika eneo la Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingra kwa Tanzania bara ni pamoja na kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa maji



kwa asilimia 83 vijijini na mijini asilimia 91, ujenzi na ukamilishwaji wa miradi ya maji ya kimkakati pamoja na kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji.

# Tanzania na Ujerumani zimedhamiria kuendelea kuhifadhi maeneo oevu.



Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Maji na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) zimesaini mkataba ili kutekeleza Mradi wa Uhifadhi wa Maeneo Oevu na Bioanuwai ya Kidakio cha Katuma, Mpanda

Mradi wa IKI Katuma utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kwa gharama ya kiasi cha Euro 4,000,000.00 zitakazotolewa na Serikali ya Ujerumani.

Lengo la mradi IKI Katuma ni kuzijengea uwezo taasisi mtambuka za Sekta ya Maji katika kuimarisha ushirikiano na kubadilishana maarifa ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji ili kuhakikisha huduma za mifumo ya ikolojia zinatumika kwa maendeleo endelevu.



# Sekta ya Maji yazidi kushirikiana na wadau wa kimataifa kuimarisha huduma

Serikali imekutana na ujumbe kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Asasi ya Kimataifa ya Water Aid lengo likiwa kuimarisha Sekta ya Maji kusonga mbele zaidi katika kutoa huduma kwa wananchi.



Kikao kimeongozwa jijini Dodoma na Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri pamoja na Menejimenti ya Wizara ya Wizara ya Maji.
Kikao kimefanyika ikiwa ni takribani miezi miwili tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupokea tuzo ya Kinara wa Maji Afrika (Pan-African water, Sanitation and Hygiene Award) kutoka asasi ya kimataifa ya Water Aid ambayo imetambua uongozi mahiri wa Rais Mhe. Dkt. Samia katika kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira nchini kwa wananchi hapa nchini.

Pamoja na hilo Mhe. Dkt. Samia katika tuzo hiyo alipewa heshima ya kuwa Mlezi wa Bara la Afrika katika Masuala ya Maji na Usafi wa Mazingira

Pamoja na hilo, Siku ya Maji Duniani Machi 22, Rais Mhe. Dkt. Samia alipewa tuzo ya Kitaifa ya Mageuzi katika Sekta ya Maji (Game Changer Award).





Gemma Querol Prades ambaye ni kiongozi Mkuu upande wa Maji, Usafi wa Mazingira na usafi Binafsi kutoka UNICEF katika kikao amesema serikali ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya sekta ya maji na kwamba UNICEF ipo tayari kushirikiana na Tanzania katika kuhakikisha maendeleo zaidi yanapatikana katika huduma ya maji.

# TEHAMA Maji watakiwa kuhakikisha mifumo inasomana

Wataalamu wa TEHAMA katika Sekta ya Maji wametakiwa kuongeza nguvu katika kuhakikisha mifumo ya kidigiti inasomana kuendana na teknolojia inavyokua.
Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amesema hayo Mtumba, jijini Dodoma na kuongeza kuwa hatua hiyo itarahisisha kupata taarifa mbalimbali kuhusu huduma ya maji kwa haraka.




Akiongea na wataalamu hao amewataka kutafuta namna bora itakayowezesha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu masuala ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kupitia mifumo.



“Hakuna sababu ya kuanza kuzitafuta taarifa za hali ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwenye makaratasi au kwa watu,haya yanaweza kufanyika kupitia mifumo iliyo jitosheleza.” Mhandisi Mwajuma amesema.
Pamoja na hilo, awamewapongeza wataalamu wote kwa jitihada wanazo zifanya katika kuhakikisha lengo na mkakati wa Wizara ya Maji yanafanikiwa kupitia TEHAMA.

# Elimu zaidi kuhusu mazingira, mabadiliko ya tabianchi na biashara ya hewa ukaa yatolewa kwa wataalamu wa serikali



Wizara ya Maji imejipanga kujenga uwezo wa Kitalaamu ili kuimarisha mikakati katika kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akiongea kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji jijini Arusha, Mkurugenzi wa Uandaaji wa Miradi, Uratibu na Usimamizi wa Mazingira; Mhandisi Dorisia Mulashani pamoja na hayo akifungua mafunzo hayo ametoa wito kwa wadau wengine katika kulinda Mazingira na kutumia fursa za mabadiliko ya tabianchi na biashara ya hewa ukaa katika kupata fedha za miradi.

Amesema mafunzo hayo yatawezesha kufungua milango ya kufaidika na fedha za kimataifa kupitia biashara ya hewa ukaa.

Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto ( UNICEF) Bi. Gemma Querol ameipongeza Wizara ya Maji kwa kuandaa mafunzo hayo na kuwakutanisha wadau mbalimbali katika kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhifadhi mazingira na mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kushirikiana na UNICEF.

Mafunzo hayo yatadumu kwa siku tatu yakilenga kujenga uwezo kwa Watalaam wa Wizara ya Maji na taasisi zake kuhusu mazingira, mabadiliko ya tabianchi na fursa za biashara ya hewa ukaa (carbon trade).

Wadau wengine wanaohudhuria ni mashirika ya kimataifa ikiwamo UNICEF, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Ofisi ya Makamu wa Rais na kituo Kitaifa cha usimamizi wa hewa ukaa (National Carbon Monitoring Centre) na wawakilishi Wizara za kisekta katika kujenga uwezo na kujadili changamoto zinasababishwa na mabadiliko ya tabianchi, fursa za ufadhili wa fedha za mabadiliko ya tabianchi, pamoja na kupitia mpango ya utekelezaji wa malengo wa Sekta ya Maji ndani ya Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (NDC 3.0).







Aweso apata kifungua kinywa na wastaafu wa Maji

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), pamoja na viongozi wengine wa wizara akiwamo Katibu Mkuu Mhandisi Mwajuma Waziri na Naibu Katibu Mkuu Bi. Agness Meena wameshiriki katika chai ya asubuhi na mjumuiko wa baadhi ya watumishi waliomaliza safari ya utumishi wa umma katika Wizara ya Maji.

Tukio hilo limefanyika katika Ofisi ya Waziri Aweso, Mtumba jijini Dodoma.

Mhe. Aweso katika hafla hiyo amesema pamoja na kustaafu kwa watumishi hao, bado wao ni hazina kubwa katika Sekta ya Maji na waendelee kuisaidia jamii na serikali popote watakapokuwa katika maisha nje ya utumishi wa umma kufanikisha huduma ya maji.

Waziri Aweso pamoja na kuwatakia kheri amewakabidhi tuzo kwa umahiri na kujitoa kwao katika kipindi chote cha utumishi wao.



# Wizara ya Maji yakabidhi kisima cha maji Buigiri



Wizara ya Maji imezindua na kukabidhi kisima chenye uwezo wa kutoa maji kwa siku lita 12,000 na kuhudumia zaidi ya wakazi 120 wanaoishi katika eneo la Shule maalum ya Msingi ya Buigiri wilayani Chamwino mkoa wa Dodoma.

Kazi ya uchimbaji wa kisima hicho ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji chini ya ardhi unaotekelezwa na Taasisi inayosimamia rasilimali za maji chini ya ardhi katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC-GMI) katika nchi 16 za SADC.

Akizungumuza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali za Maji, Robert Sunday, amesema mradi huo umefadhiliwa na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kupata fedha kutoka Benki ya Dunia(WB).

Amesema hapa nchini mradi huo umetekelezwa katika kata ya Nzuguni na Buigiri jijini Dodoma na kwamba lengo la kuutekeleza ni kuendeleza juhudi za serikali ya awamu ya sita katika kuhakikisha makao makuu ya nchi yanapata maji safi na salama yenye kujitosheleza.

Ameishukuru SADC GMI na WB na wadau wote waliowezesha itekelezaji wa mradi huo ambao utakuwa na manufaa makubwa huku akisisitiza kuwa Wizara itaendelea kugusa maisha ya watu na kutimiza lengo la upatikanaji wa huduma bora ikiwemo maji safi na salama kwa ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akishiriki kikao na menejimenti ya Wizara ya Maji. Kikao hicho kimehusu masuala mtambuka kuhusu Sekta ya Maji nchini katika kuleta mabadiliko makubwa kwa wananchi na kazi mbalimbali wanazofanya za kiuchumi. Kikao kimefanyika Mtumba, jijini Dodoma










Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) na Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb) wakipongezwa mara baada ya Bajeti ya Wizara ya Maji 2025/2026 kupitishwa Bungeni jijini Dodoma.

# Msomera maji kufikishwa katika makazi

Serikali imejipanga kuhakikisha huduma ya maji inaimarishwa kwa wananchi walioamua kuhamia eneo la Msomera, Handeni.

Naibu Katibu Mkuu Bi. Agness Meena akiongea kwa Niaba ya Waziri wa Maji kuhusu huduma ya maji amesema kazi kubwa inafanyika kuhakikisha miundombinu ya maji inafika katika maeneo yote ya makazi pamoja na kujenga mabirika ya mifugo.

Amesema kazi ya ujenzi inafanyika kwa awamu na hivi sasa ni awamu ya nne, ambapo bwawa la maji la Msomera pamoja na kutoa huduma lipo katika hatua za mwisho za utekelezwaji pamoja na matanki ya ukubwa mbalimbali ya kuhifadhi maji.
Pamoja na ukaguzi wa mradi, Naibu Katibu Mkuu Bi. Meena alipata fursa ya kufanya kikao pamoja na watumishi wa Sekta ya Maji wanaoishi Msomera na kusisitiza utekelezaji wa kazi kwa ubora unaotakiwa, ambapo amewahakikishia kufuatilia masuala yote ya msingi yanayowahusu pamoja na watumishi wengine ili kazi ifanyike kwa kiwango kama Serikali inavyotaka katika kuwahudumia wananchi.
Msimamizi wa mradi wa RUWASA Mhandisi Nobert Temba ameainisha usanifu wa kazi hiyo ni uwezo wa kuhudumia bila tatizo kwa miaka 20
Bi. Meena katika ukaguzi wa kazi hiyo ameongozana menejimenti ya Wizara ya Maji, RUWASA na uongozi wa wananchi wa Msomera.
(Hivi sasa Bi. Agness Meena ni Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi)





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akifuatilia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo linafikia ukomo





Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mha. Mwajuma Waziri akiwa Bungeni Jijini Dodoma wakati wa Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kufunga Bunge la 12.



# Watumishi wajengewa uwezo zaidi kushiriki mijadala ya maji shirikishi





Watumishi wa Wizara ya Maji wakijengewa uwezo kwa kushirikiana na Taasisi ya Umoja wa Mataifa ya Chuo Kikuu cha Maji, Mazingira na Afya (UNU - INWEH) kuhusu kushiriki katika vikao na mijadala ya maji shirikishi (Maji ya kimataifa).

Mafunzo yamwfanyika Mtumba, jijini Dodoma ambapo Tanzania inatarajia kuwa mratibu wa mafunzo ya masuala ya maji shirikishi kwa nchi za Afrika.

Wiki ya Mazingira , Jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Uandaaji wa Miradi, Uratibu na Usimamizi wa Mazingira Wizara ya Maji Mhandisi Dorisia Mulashani akiwa katika banda la Wizara ya Maji akiangalia masuala ya elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu utunzaji wa mazingira










Menejimenti na watumishi wa Wizara ya Maji wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi. Mwajuma Waziri wameungana na ndugu, jamaa, marafiki na viongozi mbalimbali kutoa pole na faraja kwa familia ya Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) katika Hitma ya mdogo wake Mhe. Aweso, marehemu Ally Hamidu Aweso (Mb) , aliyefariki ghafla akihudhuria Bajeti ya Wizara ya Maji jijini Dodoma.

Hitma hiyo imefanyika Mkoani Tanga, wilaya ya Pangani

Safari ya mwisho ya Ally Babu Aweso, mdogo wa Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ikihitimishwa Pangani, mkoani Tanga. Marehemu alifariki wakati wa Bajeti ya Wizara ya Maji Jijini Dodoma.
Wandaji wa Jarida hili tunatoa Pole kwa Mhe. Aweso, familia, ndugu, jamaa, marafiki na wadau wote. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe pumziko la amani na milele mpendwa wetu Babu, hadi wakati mwingine. Amina.



**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz